

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA



BODI YA WATAALAMU WA UNUNUZI NA UGAVI



TAARIFA KWA UMMA

ORODHA YA MAJINA YA WATAALAMU HAI WALIOSAJILIWA NA PSPTB

Dodoma Oktoba 28, 2026.

Bodi ya wataalam wa ununuzi na ugavi (PSPTB) ni taasisi ya serikali iliyopo chini ya wizara ya Fedha, iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi, Sura ya 179. PSPTB inamamlaka ya kusimamia na kudhibiti viwango vya kitaaluma, mwenendo na maadili ya kitaaluma katika taaluma ya ununuzi na ugavi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa mujibu wa kifungu cha 7(g) cha Sheria husika, Bodi hii imepewa mamlaka ya kipekee ya kusajili watu waliokidhi vigezo vya kitaaluma na kuwapa mamlaka ya kisheria ya kufanya kazi za kitaalamu katika tasnia ya wataalam wa ununuzi na ugavi.

Kwa mujibu wa kanuni ya 37(3) ya kanuni za Bodi ya wataalamu wa ununuzi na ugavi za 2009, PSPTB inatoa rai kwa waajiri wote wa sekta za umma na binafsi kuhakikisha kuwa kazi za ununuzi na ugavi zinafanywa na wataalamu ambao majina yao yamewekwa kwenye tofuti ya PSPTB na sio vinginevyo.

Hata hivyo, orodha iliyowekwa kwenye tovuti ya PSPTB ni ya wataalamu hai waliosajiliwa na PSPTB hadi kufikia tarehe 18/10/2026. PSPTB itaendelea kuhuisha majina ya wataalamu wa ununuzi na ugavi kwa kadiri watakavyokidhi vigezo. Kwa changamoto yoyote tafadhali wasiliana na PSPTB kwa simu namba **0738 441 971** au **0737 157312**.

Imetolewa na :

Digitally Signed By Alex Donald
Mfungo
Wed Oct 28 15:55:54 EAT 2026

Alex Donald Mfungo
For :EXECUTIVE DIRECTOR